# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 5, Mei 2019

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

Mhariri

## Kukutana na yule aliye na hitaji



Katiba ya ASC, ikiongea juu ya utambulisho wetu wa Utume, inatukumbusha kuwa, katika kuwa wazi kwa mwingine, katika ushuhuda wa Upendo wa Mungu na zaidi ya yote katika kujitoa kwa maskini na waliotengwa, tunatekeleza utume wetu wa kushiriki katika kazi ya ukombozi ya Yesu Kristo.

Katika maisha ya Waabuduo kukutana na masikini, wasio na sauti, wasiofahamika, inamaanisha kugundua uso wa Kristo. Ni masimulizi mengi ambapo kila siku tunakuwa ushuhuda. Masimulizi ya udhaifu wa kibinadamu, ya umasikini, ambayo huwa matukio ya Ufufuko. Maisha yetu yaliyotolewa, yako wazi kwa utafiti, kwa mapokezi, kwa kusikiliza ule uso ambapo tunamwona Yesu aliyejeruhiwa, aliyechafuliwa, aliyeachwa, au aliyehuzunishwa, yanakuwa ni mazingira ya teolojia ya kukutana, utunzaji wa aliyejeruhiwa na uwepo wa kirafiki ambao unaleta tumaini kwa ajili ya wale ambao wanateseka kwa upweke.

Katika idadi hii, kwa namna ya pekee, simulizi la mang'amuzi ya Serafina Cinque na la Masista, Iolanda na wengine, wanashuhudia kuwa Roho anatutakatifuza katika huduma inayotolewa kwa furaha na unyenyekevu, akitufananisha zaidi na Kristo Msulubiwa na Mfufuka.

Hata Papa Francis, wakati wa ziara zake za mwisho za kichungaji katika nchi za Kiarabu, alisisitiza tunu ya upendo wa kidugu wa kiutu kama njia pekee kwa ajili ya amani ya dunia na ya kuishi pamoja, mlango pekee kuelekea wakati ujao; haki iliyo na msingi katika huruma ni njia ya kufuata ili kufikia maisha ya heshima ambayo ni haki ya kila mtu.

Injili za siku hizi, zenye hadithi tofauti za kibinadamu za Yesu, zilizoundwa na kukataa kupokea, magonjwa na uponyaji, zinatusindikiza katika safari ya maandalizi ya Pasaka, tunaalikwa kwenye mabadiliko. Neno la Mungu linatukumbusha kuwa hakuna maisha bila kukutana, hakuna tumaini jipya kwa mwanzo mpya kama si katika kupokeana ambako huponya. Haisaidii kubaki kunaswa katika majonzi tasa, bali kuwa kama buu, ambalo hutoka kwenye kijumba chake cha nyuzi, ili kujibadili kuwa kipepeo na kutandaza mabawa yake yenye rangi ya kupendeza ya kwanza. Msamaha wa Yesu uliotolewa kwa mkosefu unashuhudia kuwa Yeye alikuja ili katika Yeye peke yake tupate mwanzo mpya na kila mtu apate fursa ya maisha mapya.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Mhutasari

*Mhariri*
◇ Kukutana na yule aliye na hitaji 1
*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
◇ Mang'amuzi ya ziara ya kichungaji 2
*Toka Ulimwengu ASC*
◇ Ndoto inaendelea… 5
◇ Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke, 2019 6
◇ Nyimbo, kichekesho na Fumbo la Pasaka 7
◇ Damu ya Kristo mto wa rehema, utuokoe 8
◇ Miaka 185° Kumbukumbu ya kuanzishawa Shirika 9
*Nafasi JPIC/VIVAT*
◇ "Tunataka kuwa sauti ya asiye na sauti" 10
*Ndani ya Shirika*
◇ Kalenda ya Uongozi Mkuu 11
◇ Sikukuu za kuzaliwa 11
◇ Maadhimisho ya nadhiri za kitawa 11
◇ Waliorudi Nyumbani kwa Baba 11

# Mang'amuzi ya ziara ya kichungaji

*Masista wa Region ya Zagabria*
*Wanashirikisha kwa hiyari Shirika zima*
*Mang'amuzi yao ya ziara ya kichungaji 2019*

Nimeishi muda wa zara ya kichungaji kama kawadi ya pekee ya Mungu. Mkuu wa Shirika na Halmashauri yake, kwa heshima na upendo wametuonyesha mambo ambayo hayaendi vizuri na yale tuanayoweza kuboresha. Mabadiliko yanahitaji uvumilivu.
Yote kidogokidogo hukua, lakini Mungu tu ndiye anayekuza. Katika ziara hii ya kichungaji nimefaidika na upendo na juhudi na nilishiriki katika mikutano kwa moyo wazi. Nimeonja unyenyekezu na faraja. Sisi sote tuligundua utofauti lakini pia mambo ya kawaida. Nilihisi kuwa kila sista ni wa muhimu, maoni yake na hisia zake. Sisi sote tulipata muda wa kutosha kujieleza wenyewe. Katika hali ya uaminifu tumeamua mambo tunayotaka kufanya. Hizi ni hatua ndogo lakini wazi na zenye uhakika, zitatusaidia sana kukua katika jumuiya. Ninaushukuru Uongozi Mkuu kwa ajili ya maandalizi yake na muda uliotolewa kwa ajili yetu, kwa unyofu wake, unyenyekevu, upendo, hali halisi ya kujali maslahi ya kila sista.

***Sr. Katica Tušek, Banja Luka***

Kwa kweli, niliishi ziara hii kama "mkutano". Ijapo najua kuwa yalikuwa yamendaliwa (vitu, kazi, muda kwa ajili ya kufanya kazi binafsi na za pamoja, mashirikisho, ...), kwangu ilionekana kama yote yalikuwa yanaenda kwa utaratibu na kwa hiyo yote yalikuwa mazuri na yenye utajiri.

***Sr. Marija Bilanović, Zagreb, Miramarska***

Nilifurahi sana na nilishangaa maandalizi yao na kazi iliyofanywa na Uongozi wetu Mkuu. Yote yalikuwa yenye utajiri. Nilifuraha kwa kuwa Uongozi Mkuu umetembelea Jumuiya yetu ya Ražanac. Utukufu kwa Damu ya Kristo!

***Sr. Ana Iveljić, Ražanac***

Nimeishi ziara hii kwa mguso mkubwa. Nimeguswa na unyofu wao na mbinu yao. Mpango, wenye mambo mengi, ulifuatwa vizuri na kwangu, Mwabuduo Damu ya Kristo, nilifarijiwa. Mkuu wetu wa Region, Sr. Ana Marija Antolović, alitafsiri viruri, kwa utulivu na umakini.

***Sr. Virginija Kolić, Bjelovar***

Mkutano na Uongozi Mkuu umenifanya nionje umoja, utofauti, kupitia tamaduni tofauti na alama za Karama ya ASC. Nilistaajabia mitindo na utajiri wa kuishi Injili katika hali tofauti na utume. Namshukuru Mungu kwa utajiri wote ambao "nimeuweka moyoni mwangu" na ninamwomba neema na nguvu ili kuuishi katika maisha ya kila siku.

***Sr. Benita Antolović, Vrsar***

Nilitiwa moyo na ziara ya masista kupitia mikutano yote ambayo tumeifanya. Nasonga mbele kwa hamu mpya ya kuimarisha tasaufi ya ASC na umoja pamoja na masista wote na wapendwa wangu wote.

***Sr. Ljubica Radovac, Okučani***

# Nafasi kwa Uongozi Mkuu

Ziara ya Kichungaji toka mwanzo wake imenijaza uhai. Tumepata mang'amuzi yenye utajiri na fursa ya kukua. Tunashukuru kwa safari ambayo kwayo tunajisikia kuchangia kwenye utajiri wa Kanisa. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kushuhudia uso wa Mungu katika jumuiya, kwa watu ambao tunafanya kazi nao na wale tunaokutana nao. Mada ya ziara imetupa mtazamo wazi wa kile kinachotakiwa kuwa matindo wa maisha yetu. Shukrani kwa Uongozi Mkuu kwa kutupa muda wa kuwa pamoja na wa kujali.

***Sr. Ljubica Šumić e Sr. Severina Šokić, Bihać***

Ninapofikiri tena mkutano pamoja na Uongozi Mkuu moyo unajaa shukrani, na ninakosa maneno ya kueleza yote yale ninayojisikia. Kazi, ishara, picha, yote yamechorwa moyoni mwangu na imenipa nguvu mpya kwa ajili ya maisha ya kila siku. "Mioyo katika Umoja, Injili katika Ulimwengu", ni mada iliyo wazi sana na ya sasa na kila mara inarudisha kwenye kumbukumbu siku za mkutano wetu, kwenye yale tuliyoshirikishana pamoja. Ninawashukuru masista kwa namna ya pekee kwa ajili ya hali nzuri ambayo ilijengeka kati yetu, uwazi, uhuru wa mazungumzo, uelewa. Kwa namna hiyo mabawa binafsi na yale ya wote kwa ajili ya ndoto zetu yanakua. Kwangu yalidhihirika maamuzi binafsi kufuatana na mkutano wa kikundi. Kwa uwajibikaji nitajaribu kuyaweka katika matendo ya kila siku, maamuzi ambayo yanawakilisha tunda la kweli la kukutana. Kwa ajili ya hili na kwa yote ninamshukuru Mungu kwa namna ya pekee na masista!

***Sr. Sunčica Kunić, Zagreb, Miramarska***

Wazo ambalo liliniongoza wakati wa ziara ya kichungaji lilikuwa ni aya ya Maandiko Matakatifu Fil 2,2-5 (Mioyo … katika Umoja: Injili katika Ulimwengu …). Tulifanya kazi za binafsi na za vikundi kwa mabadiliko hai sana, mara nyingi yanayoonekana katika hali za maisha. Masista wengi walishiriki na walitaka kujieleza. Mpango ulijumuisha nyakati za kufanya kazi kwa kutumia alama. Kwangu haya yalikuwa mawasiliano ya kweli ya Picha ya umoja inayoelezwa kwa namna iliyo halisi zaidi na ya ubunifu. Mang'amuzi ya kimataifa kwangu ni utajiri ambao unaumba mang'amuzi mapya na mawazo mapya ya karama ya umoja. Ujumla wa upendo mkombovu wa Mungu unaoshinda picha za watu, tamaduni na dini kwa sababu hugusa kila mtu. Upendo wa Roho Mtakatifu ulimiminwa ndani ya watu wote ili kuwafunga na kuwapokea katika chemchemi ya kweli ya Upnedo, ndani ya Baba.

***Sr. Ankica Klepić, Zagreb, Trešnjevka***

Ziara ya kichunga ilifanyika katika hali ya uwazi na ya utaratibu, shukrani kwa kazi ya maandalizi yaliyofanywa kabla na kwenye maandalizi ya mikutano. Nilisikia kuwa katika kukaa kwetu pamoja, katika umoja wetu "tumekusanya" pamoja na Yesu katika shamba la mang'amuzi yetu ya maisha binafsi na ya pamoja. Roho Mtakatifu alikuwa katika utendaji na aliongea kwa kupita mdomo wa kila mmoja wetu. Mashirikisho na kusikiliza wengine yalinisaidia kwa urahisi kusoma upya mitazamo yangu, kueleza mang'amuzi yangu na hali zangu, na kujikumbusha kile ambacho ni muhimu.

***Sr. Jadranka Obućina, Sarajevo***

Wote katika hali ya furaha na ya matazamio, tulikuwa tayari kusikiliza kile anachotuambia Bwana kupitia ziara ya kichungaji "Mioyo... katika ushirika: Enjili katika Ulimwengu". Katika kipindi cha tafakari binafsi na ya kikundi, wakti wa mashirikisho ya mang'amuzi, tulisikia mwaliko wa kukua kiroho katika furaha, amani na hamu ya kukua ili kuwa... nia ambayo ilikuwemo ndani ya Kristo Yesu (Fil 2,3).


***sestre iz zajednice Nova Topola***

Kwangu ziara ya kichungaji ilikuwa ni mang'amuzi mazuri ya ushirika. Imenifariji kwa ajili ya safari endelevu ya imani na imenifanya kwa kiasi kikubwa kuelewa kuwa yale yote ninayofanya ni kwa ajili ya ukuaji wa Shirika. Nimeshangazwa kwa utayari wa Uongozi Mkuu katika kumsikiliza kila sista; wametoa muda kwa kila mmoja na wamejifumza majina yetu. Ilikuwa kazi lakini yenye kuzaa matunda.

***Sr. Zvonimira Borščak, Zadar***








Knjižnica Sv. Josip


















DOM DRAGI BLIŽNJI



Eneo la Bara: Amerika
Region ya Manaus

## Ndoto inaendelea…

Tangu miaka ya 1970, Sista wetu Serafina Cinque alikuwa ameanza kuwakaribisha wanawake wajawazito wa Transamazzonica ambao hawakuwa na nafasi ya kujifungua, na hata leo kutafuta msaada kunaendelea katika nyumba ya Divina Providenza, inayoendeshwa na Masista Waabuduo wa Damu ya Kristo, katika miaka hii ya mwisho ilikuwa chini ya uongozi wa Sista Zélia Valentim, ASC.

Ndoto ilidhihirika kwenye mwaka wa 1980, inajumuisha sehemu tatu:

1- "Rifugio San Gaspare" ambayo inapokea watu ambao wana mahitaji ya ushauri wa kitabibu na vipimo vya kimaabara, yenye nafsi ya vitanda 60. Nyumba hii daima imejaa watu wanaokuja kutoka sehemu zingine ambao hawana uwezo wa kifedha kwa ajili ya kulipia malazi. Hapa wanapokea mahitaji muhimu, kufua, kuoga, wanapata usafiri kwa ajili ya kwenda hospitali na wanaweza kupata milo mitatu: kifungua kinywa, chakula cha mchana, cha usiku na kinywaji na vitafunwa muda wa alasiri.

2- Nyumba ya "Divina Providenza" ambayo inapokea wanawake wajawazito walio na matatizo makubwa, hata wao hawana uwezo wa kulipia matibabu. Kila mmoja analeta msindikizaji anayebaki naye hospitalini kwa ajili ya kujifungua na siku zinazoendelea.

3. Makazi ya Maista Waabuduo, daima yako wazi kwa ajili ya kupokea watu wanaoomba na hasa wafanyakazi ambao wanafanya usafi wa nyumba zote tatu, wangoja mlango, wa bustanini na wa bustani ya mboga, wa jikoni na wa dobini. Kuna walinzi wa usiku kwenye nyumba zote tatu. Felipe, dreva, kwa siku nzima anasindikiza wagonjwa ambao wanahitaji kusafiri kwa ajili ya vipimo mbalimbali.

Huduma zote za kiuguzi ziko chini ya uangalizi wa muuguzi Regina anayejitolea kwa tabasamu daima akiwa tayari kujibu na kuwahudumia wote wale ambao wanahitaji msaada wake.

Siku zote baada ya kifungua kinywa, wageni wa Rifugio na wanawake wa Nyumba ya Divina Providenza, na wafanyakazi na masista wanaenda kanisani ili kusali Sala ya asubuhi na kufanya tafakari ya Enjili ya siku.

Kila Alhamisi, Mmisionari CPPS, Padri Lucas Fuertes, anaadhimisha Misa saa 15.00. Jumapili, wageni Wakatoliki (wengi ni wa dini nyingine), wanawake wajawazito pamoja na masista ASC hushiriki Misa katika Paroki ya Mama wetu Mkingiwa dhambi ya asili ambapo, juu ya madhabahu ya kanisa upande wa kulia, yamehifadhiwa mabaki ya mwili wa mtumishi wa Mungu Serafina Cinque.

Tunaona jinsi Mungu alivyokaribu nasi shukrani kwa maombi ya mtumishi wa Mungu Serafina: kwa kweli tunaendelea kupokea mchango wa chakula na mavazi. Pia tulifungua duka ndogo ambapo watu masikini wanaweza kununua bidhaa kwa bei wanayoweza kulipa, chini ya uwajibikaji wa Bibi Vilma. Mapato yatokanayo na uuzaji hugharamia matengenezo ya nyumbani.

Siku moja hatukuwa na nyama ya kupika, kwa mshangao alikuja bwana mmoja ambaye alituletea ng'ombe mzima aliyechinjwa na siku hiyo hiyo mtu mwingine alitoa nusu ya ndama ambayo angepaswa kuchinjwa; hii imekuwa ikitokea kwa miaka. Maduka makubwa hutuma matunda, mboga mboga na kila aina ya chakula na kamwe Mungu Mpaji hatuachi tukose mahitaji ili kukidhi mahitaji yetu. Huu ndio muujiza mkubwa wa Mtumishi wa Mungu Serafina: kuendelea kuhamasisha mioyo ya wale walio na mali kuwasaidia wasio na kitu.

Nilizaliwa karibu na mto Juruá, mojawapo ya makabila ya Amazoni, na ninajua aina kuu za samaki wanaopatikana huko, lakini nilishangaa siku moja ambapo polisi alikuja kutuleta tani tatu za samaki waliotaifishwa kwa sababu walivuliwa nje ya msimu wa uvuvi. Masista walishirikisha hii mali kwa wafanyakazi wote na taasisi zingine zinazotoa huduma za upendo. Ukarimu wa watu ni wa kushangaza. Hatupokei msaada wowote kutoka kwenye taasisi mahalia au za taifa. Ni wazi kwamba Bwana anaendelea kusikiliza sala za maombi za mtumishi wa Mungu Serafina. Ni nini kinachokosekana kwa ajili ya kutangazwa kwake mtakatifu?

***Sr. M. Clara de Albuquerque Silva, ASC***







Eneo la Bara: Asia
Region ya India

# Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke, 2019

## Mysuru & Tarikere – India

Tarehe 8 Machi 2019 katika vituo vyetu vya kijamii huko Mysuru na Tarikere ilisherehekewa Siku ya Kimataifa ya Mwanamke, kwa lengo kuu la kuwaelimisha wanawake juu ya nafasi yao katika jamii.



Zaidi ya wanawake elfu moja walishiriki sherehe kutoka vituo vyote viwili vya kijamii vya Mysuru na Tarikere vinavyoongozwa na Masista Waabuduo Damu ya Kristo. Mpango mzima umewasaidia wanawake kuona usawa wakitiwa moyo kujenga maisha wakifuata mfano mmoja. Ili kuboresha maisha yao na kuthamini vipaji vyo, tuliandaa mashindano ya michezo na tamaduni, wengi walishiriki na kuthani tukio hili. Ili kuhimiza na kuthamini Makundi ya Sangas ya Misaada - Misaada ya wanawake, vilichaguliwa na kupewa zawadi vikundi bora, vikundi vya utamaduli vilijieleza kwa ngoma na nyimbo, wakionyesha vipaji vyao.





Wanawake na wasichana wengi wanathamini vituo vyetu vya kijamii, kwa kuwa wanafunzwa mambo mazuri ili kukabiliana na maisha. Programu mbalimbali zinawawezesha kuwa mabinti, dada, wake na mama wazuri katika familia zao na hivyo kujenga jamii bora. Vituo vyote vya kijamii viliufuata mpango mzima kwa vizuri na mafanikio yaliyopatikana yanahusishwa na kazi ya ushirikiano wa watu wengi, hasa jumuiya za masista za Aradhana, wa kituo cha kijamii cha Navodaya huko Mysuru, wa kituo cha kijamii Navajeevan Tarikere na Maria Nilayam Kituo cha kijamii katika Velugodu. Asanteni nyote.



***Sr. Jaicy Karukuttikaran, ASC***

Eneo la Bara: Ulaya
Region ya Italia

# Nyimbo, Kichekesho na Fumbo la Pasaka



Hivi ndivyo siku ilivyotukia.

Tarehe 23 Machi, Roma, kwenye baraza kuu la SSD, Monica Brown, mtu maarufu wa Australia na Hilary Musgrave, mchekeshaji wa Irland, waliongoza siku ya tafakari ya kina ya kwaresima kwa ajili ya watawa wanaoongea lugha ya kiingereza. Mada ilikuwa "Kurudi" – zawadi ya mabadiliko. Walishishiri masista zaidi ya 140 wanaotoka Iraq, Ufaransa, India, Indonesia, sehemu mbalimbali za Afrika, Amerika Latin na sehemu zingine, kwa hiyo kiingereza kilizungumzwa kwa lafudhi mbalimbali.

Fumbo la Pasaka lilikuwa ufunguo wa somo la tafakari. Monica, katika mada yake aliunganisha Maandiko Matakatifu na mziki, mashirikisho, pamoja na simulizi na nyakati za ukimya. Hilary, mchekeshaji wa Nafur, aliwasilisha mada inayohusu, upendo, uchaji, heshima, moyo kama wa Mungu.

Monica alimzungumzia Kristo wa Ulimwengu, wa mafunuo mawili ya Mungu, wa kwanza katika Uumbaji na wa pili katika Kristo, na kwamba umwilisho wa Yesu katika mpango wa kwanza wa Mungu, ungefanyika kutokana na upendo safi, kumfunua Mungu wa Upendo kwa binadamu. Ujio wa Yesu siyo wa pili kwa dhambi ya asili, kwa sababu haukuwa suala la malipo na fidia. Yesu hakutumwa na Baba kuteseka na kufa, ili kupata haki yetu. Alikuja, ili kufunua upendo mkubwa, wa Mungu, upendo wa Muumba wetu ambaye alitaka kuwa na sisi na kwa hiyo akawa mmoja wetu. Yesu kwa umwilisho wake alikuwa mwanadamu kabisa, na kama tulijaribu kumkataa, wiki nzima Kuu ingekuwa haina maana.

Fumbo la Pasaka ni kiini cha maisha yetu ya Kikristo. Sisi tunabusu msalaba kwa upendo na heshima wakati tunapoheshimu mateso ya Yesu na ya binadamu. Wokovu sasa unapita kwetu wakati tupo, tuungane na watu wanaoteseka. Kwa utulivu na hisia za ndani kabisa, sisi watawa ni uwepo unaofariji wa Mungu kwa ajili ya wale walio katika mateso. Tumepewa uwezo wa kuleta mabadiliko. Mungu hutoa nguvu kwa ulimwengu kwa ujumla, akiuwezesha kuendelea wenywe, kujidhihirisha na kujitokeza kwa uhuru. Neema siyo kitu tu. Neema ni uwepo wa Mungu. Ufufuko ni kielelezo cha kiini cha upendo wa Mungu anayejitoa mwenyewe.

Kipindi cha Kwaresima tunatafuta kurudi ndani yetu wenyewe na hivyo kurudi nyumbani – kwenye mikono ile ya upendo usio na masharti.

***Sr. Marcia Kruse, ASC***

# Damu ya Kristo Mto wa Rehema, utuokoe



Napenda kuwashirikisha masista mang'amuzi ya huduma yangu kwenye Nyumba ya Yatima kwenye Kituo cha Matunzo na cha Mafunzo huko Wrocław. Nilianza kazi hii ya mafunzo tarehe 1 Oktoba mwaka uliopita.

Mwanzoni mwa kazi, uwepo wangu kama matawa, ulikuwa msahangao kwa wafanyakazi wote na wazazi waliokuwa wanatembelea Nyumba ya Yatima. Baada ya muda, naona walizoea. Ingawa tunu za kikiristo zinapendwa, hata hivyo unaweza kukutana na ukosefu wa mang'amuzi ya imani, kwa namna ya pekee kati ya wageni.

Kila mara ninapokwenda kazini, ninajua kuwa ninaingia katikati ya umasikini wa kibinadamu. Tunaona mateso bila kosa, matokeo ya ukosefu wa watu waliokaribu zaidi. Watoto wote wako pamoja kwa sababu wanajikuta kwenye nyumba ya Yatima usiku na machana kwa masaa 24, lakini historia ya makazi yao hapa ni tofauti. Kwa sasa kila mtoto angalau ana mzazi mmoja. Zaidi ya yote, jambo la kusikitisha ni kwamba, kwa sababu ya kutojali, mashaka, mkato wa tamaa au mazoea, kwa kawaida wazazi wanaacha kupambana kwa ajili ya kurudi nyumbani watoto wao.

Nyumba hii ya yatima ni nafasi ya muda, hivyo watoto wako hapa kwa muda, ni kwa muda maalum tu. Baadhi yao wapo hapa kwa muda zaidi, wakisubiri kwamba hali ya matatizo iliyojitokeza katika nyumba zao itatuliwe na wazazi kufanya mabadiliko. Watoto wengine wako hapa kwa muda mrefu na, wakati panapokuwa hakuna matarajio ya kurudi nyumbani, wanandikishwa kwa ajili ya msaada au kwa ajili ya kuchukuliwa na familia nyingine.

Kuna makundi matatu yenye umri tofauti: wachanga (5), watoto wenye umri kuanzia miaka 2 -5 (15) na wakubwa zaidi kuanzia miaka 6 hadi 14 (8). Walimu wanawekwa kwa makundi maalumu, kwa sababu idadi ya watoto hupadilika mara nyingi, na zamu za kazi zinapangwa kadiri ya mahitaji.

Watoto wanateseka sana na mara nyingi wanaasi, wanahisi hasira na chuki wakati wanapopelekwa mbali na familia zao. Kwa hiyo, vitendo mbalimbali hufanyika ili kuwatuliza na kuondoa wakati huu mgumu kwa namna ambayo haiwadhuri. Mipango mingi ya kisanii, elimu na michezo inatekelezwa ili kuwapa watoto fursa nyingi za ukuaji na nafasi za maisha bora zaidi. Hata hivyo, vivutio vingi haviwezi kuwapa kile kilicho muhimu zaidi na kile ambacho kingewazezesha kupata mang'amuzi: zaidi ya upendo wa familia.

***Sr. Beata Płowaś, ASC***



# Miaka 185° Maadhimisho ya kumbukumbu ya kuanzishwa shirika

Mwaka huu tarehe 4 Machi, katika tukio la maadhimisho ya miaka 185° ya kuanzisha Shirika, tulisherehekea kwenye parokia ya Damu Azizi ya Orcasitas – Madrid, kwa adhimisho la Misa iliyoongozwa na Wamisionari wa Damu Azizi, ambayo ilihudhuriwa na jumuiya ya parokia.

Tulianza sherehe tukimshukuru Mungu kwa ajili ya uhai wa Shirika letu, tukitumia fursa hii kukumbuka wakati uliopita kwa shukrani, kuangalia wakati uliopo kwa upendo na kupokea wakati ujao kwa matumaini.

Ndoto ya Maria De Mattiasi inaendelea katika maisha na katika wajibu wa kila mmoja wetu aliyeitwa kuwa Mwabuduo Mtume wa Damu Azizi.

Ilikuwa tarehe 4 Machi wakati Maria De Mattias alipoanza utume wake. Kifuatacho ni kile anachotusimulia Yohane Merlini, kiongozi wake wa kiroho, kwa miaka 42.

“Ilikuwa Machi 1, 1834, Maria alikuwa ametimiza miaka 28 na kwa miaka kumi alikuwa akisubiri siku hiyo. Padre Biagio Valentini aliwasili Vallecorsa akimleta Maria baraka ya Gaspari del Bufalo iliyotamaniwa, pamoja na barua yake ambayo “aliitoka kwa ajili ya kuhimiza kumtegemea Mungu, ili kila kitu kifanikiwe” ... Katika safari ya Acuto, Maria alisimama Ferentino kumsalimu Askofu na kwa wazi alisema: “Monsignore, ninakwenda kwa furaha Acuto, kwa sababu utii unaniamuru, lakini siyo tu kwenda kufundisha katika shule, lakini kuanzisha Shirika” ... Machi 4 ni siku ya kwanza ya novena kwa Mtakatifu Francis Xavier, mlinzi wa Shirika jipya, walianza kazi ya Mungu. Hii ilikuwa siku ya kuzaliwa ya Shirika la Waabuduo Damu Azizi “.

Kwenye Misa tuliwakumbuka Waabuduo wote waliotawanyika ulimwenguni na pia wale ambao tunashirikishana nao maisha yetu kwa miaka mingi.

Baada Misa Takatifu ulifuata muda wa mlo wa pamoja na watu waliotusindikiza na kwa furaha tulizima mishumaa iliyokuwepo juu ya keki.







***Sr. Teresa Montiel, ASC***

# "Tunataka kuwa sauti ya yule asiye na sauti"

Siku moja ya baridi, mwanamke kijana aligonga mlango wetu hapa Dokszyce, Bielorussia. Daktari alikuwa amemtuma ili kufanya mazungumzo na Padri Andrzej. Jina lake ni Svetlana.

Tayari tangu mwaka moja sasa katika mji wetu kumekuwa na desturi kwamba wanawake wajawazito ambao wanataka kutoa mimba hutumwa na daktari ili kuongea na padri au mtu ambaye anaweza kutoa ushauri kwa ajili ya kulinda uhai.

Yote ilianza miaka miwili iliyopita katika jumuiya yetu wakati wa mkutano uliofanyika kuhusu mada ya afya, siku ya Mt. Luke. Svetlana alikuja kwetu kwa sababu hiyo na kwa kuwa alipaswa asubiri, tulipata fursa ya kuzungumza naye na kufahamu habari zake. Msichana alikuwa akiishi na baba yake katika kijiji cha Kamajsk katika hali ngumu, mama yake alifariki yeye akiwa na umri wa miaka 15 na baba yake alipoteza sheshima ya kuwa mzazi kwa sababu ya ulevi. Baada ya kuhitimu elimu ya sekondari, alikamilisha kozi yake ya kitaaluma kama mtunza bustani, kisha akapata kazi katika kampuni ya ujenzi huko Dokszyce, akiishi katika hosteli, lakini miaka miwili baadaye aliacha kazi yake kwa sababu ilikuwa nzito mno kwake, akapata kazi nyingine ya usafi katika nyumba ya uuguzi kwa miezi sita.


Jumapili moja alikwenda kumtembelea baba yake na kikundi cha wanaume waliingia chumbani mwake na kudhalilisha.

Kwa hiyo yeye hakuwa na uwezo wa kulipia hosteli kwa muda fulani, mmiliki akamtoa nje na alilazimishwa kurudi nyumbani kwa baba yake ambapo watu walipoteza heshima yake.

Alipogundua kwamba alikuwa ni mjamzito, alitaka kutatua tatizo hilo kwa kuuondoa haraka iwezekanavyo pia kwa sababu alikuwa anamwogopa baba yake na jinsi ambavyo angeweza kumtendea. Ingekuwa vigumu kumzaa mtoto na kuendelea kuishi na baba, ambaye aliendelea kunywa na kufanya fujo. Hakuwa na fedha na ili kuwa na kitu alikwenda kukusanya matunda pori na kisha kuyauza sokoni. Mchumba wake pia alitaka atoe mimba; Svetlana alikasirika na kuhisi kuwa hana nguvu. Baada ya kuzungumza na sisi na Padre Andrzej, alianza kujisikia kusita kuiondoa mimba. Tulimwalika kwa chakula cha jioni na tulimpa kitu cha kula. Alihitaji msaada, ule ambao alikuwa hajaupokea kutoka kwa dada zake wala kwa baba yake. Aliweza tu kutarajia msaada wa watu wa nje na wa watu wenye mapenzi mema.

Tulimsaidia kupata malazi na kazi za msimu kwenye hospitali. Watu wengi waliendelea kumshauri kutoa mimba, lakini aliamua kumzaa mtoto. Mamlaka ya jiji wanaamini kwamba mwanamke huyu hawezi kumlea mtoto, kwa sababu anatoka katika familia yenye matatizo, isiyo na taratibu zinazofaa. Svetlana alianza kwenda kwa mamlaka sheria kuwaomba makazi na kazi, lakini hakuna mtu aliyetaka kumsaidia. Suluhisho pekee lilionekana kuwa ni kurudi nyumbani kwa baba yake. Tuliamua kumsaidia na tukaenda kwa mamlaka ya jiji pamoja naye. Mara ya kwanza ilionekana kuwa haya yote hayakuwa na maana lakini basi kutokana na ushirikishwaji wa "wale wanaohusika" tuliweza kuingia katika mazungumzo na hivyo, waliamua kumpa malazi na kazi. Ulikuwa wakati mgumu sana, lakini watu wengine na wafadhili walianza kumsaidia: majirani, wanaparokia wetu, marafiki ... sasa ilibidi kuandaa chumba na kununua kila kitu muhimu kwa mtoto. Wakati wa kujifungua ulikuwa unakaribia. Kisha Svetlana alihitaji msaada, bila shaka alikuwa na hofu ya kumzaa mtoto, jamaa zake hawakujali maisha yake na sisi tulikuwa karibu na kumtia moyo. Mnamo Septemba 4 ajifungua mtoto wa kike aliyemwita Natalia. Hata hivyo ana wasiwasi kuwa mamlaka ya jiji watamnyang'a mtoto, kwa kuwa usimamizi bado inaendelea.

*Sr. Jolanta na masista wa Bielorussia, ASC*



# Kalenda ya Uongozi Mkuu




**2-14 Mei** Mkutano wa tume kwa ajili ya malezi
**6-10 Mei** ushiriki wa Sr. Nadia Coppa kwenye Mkutano wa UISG
**15–17 Mei** Sala ya siku tatu kwa heshima ya Mt. Maria De Mattias katika kuadhimisha miaka 185° ya kutangazwa mtakatifu
**18 Mei** Sikukuu ya Mt. Maria De Mattias
**13-18 Mei** semina kwa ajili ya wahasibu wa Shirika itakayoongozwa na Sr. Manuela Nocco
**19 Mei** maonyesho kuhusu Mt. Maria De Mattias kwenye ukumbi, yanayotolewa na kikundi cha wachezaji wa Vallecorsa
**21 Mei- 15 Juni** Halmashauri Kuu ya Shirika itakuwa Polandi kwa Ziara ya kichungaji

## *Sikukuu za kuzaliwa: tunasherehekea maisha ya:*



| | | |
|---|---|---|
| miaka 40 | | |
| **Sr. Beatrice Hillary Kimaro** | 29/05/1979 | Tanzania |
| miaka 70 | | |
| **Sr. Vladimira Galir** | 13/05/1949 | Zagabria |
| **Sr. Kris Schrader** | 14/05/1949 | USA |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Filomena De Giovanni** | 07/05/1939 | Italia |
| **Sr. Amalia Di Nunzio** | 12/05/1939 | Italia |
| **Sr. Ivana Ćerdić** | 17/05/1939 | Zagabria |
| **Sr. Leonija Ćuković** | 04/05/1939 | Zagabria |
| **Sr. Jelena Kančelarić** | 21/05/1939 | Zagabria |
| miaka 90 | | |
| **Sr. Angela Vese** | 08/05/1929 | Italia |
| **Sr. Elena Pannunzio** | 27/05/1929 | Italia |



## *Nadhiri za Kitawa*

### *17 Mei 2019*

**Nadhiri za Kwanza – Tanzania**

*Coleta John Emanuel*
*Joantha Emmanuel Mlyanga*
*Maria Anatoli Chanzi*
*Rosina Respicius Bombo*

### *17 Mei 2019*

**Miaka 25° ya nadhiri za kitawa – India**

*Sr. Mini Pallipadan (Mkuu wa Region)*
*Sr. Mini Vadakumcherry*

**Maiaka 60° ya nadhiri za kitawa – Columbia Center (USA)**

*Sr. Mary Adele Vecchione*
*Sr. Mary Peter Chiodo*

**Maiaka 65°– ya nadhiri za kitawa Columbia Center (USA)**

*Sr. Martha Wachtel*
*Sr. Mary Clare Reineberg*



## *Waliorudi Nyumbani kwa Baba*

| | | |
|---|---|---|
| 10/04/2019 | **Sr. Lucille Kerschen** | USA |
| 11/04/2019 | **Sr. Teresa Kulik** | Wrocław |
| 20/04/2019 | **Sr. Serafina Novielli** | Italia |


**Gazeti la Kimataifa**
Waabuduo Damu ya Kristo
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 5, Mei 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*